MWANGA WA ELIMU

(Imamu Muhammad Baqir A.S.)

Kimeandikwa na
Maulana Sayyid Ali Naqi Saheb

Kimetafsiriwa na
Marehemu L.W. Hamisi Kitumboy

Kimetolewa na Kuchapishwa na
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P. 20033, DAR ES SALAAM - Tanzania

MWANGA WA ELIMU
(IMAMU MUHAMMAD BAQIR A.S.)

Kimeandikwa na:
SAYYID ALI NAQI SAHEB

Kimetafsiriwa na
BWANA L. W. HAMISI KITUMBOY

Kimetolewa na Kimechapishwa na
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P. 20033
Dar es Salaam - Tanzania

Haki za kunakili imehifadhiwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania

ISBN 9976 956 03 7

Toleo la kwanza 1986, Nakala 20,000
Toleo la Pili 2007, Nakala 1,000

Kimetolewa na Kuchapishwa na:
BILAL MUSLIM MISSION OF TANZANIA
S.L.P 20033
DAR ES SALAAM - TANZANIA

MWENYEZI MUNGU ANASEMA:

يَوْمَ نَدْعُو كُلَّ أُنَاسٍ بِإِمَامِهِمْ ۖ فَمَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَأُولَـٰئِكَ يَقْرَءُونَ كِتَابَهُمْ وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٧١﴾

(Ewe mwanadamu! Ikumbuke) siku Tutakapowaita kila watu pamoja na Imamu wao; basi atakayepewa kitabu (chake cha Amali) kwa mkono wa kulia, hao watavisoma vitabu vyao (kwa furaha); ...

(Bani Isra'il, 17:71)

MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.) AMESEMA:

من مات و لم يعرف إمام زمانه، مات ميتة جاهلية

"Yeyote yule afaye pasi na kumjua Imamu wa zama zake, atakuwa kafa kifo cha ujinga".

MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.) AMESEMA:

"Hao (Ulul Amr watajwao mwenye Qur'ani 4:59) ni Makhalifa wangu na Maimamu wa Waislamu baada yangu. Wa kwanza ni Ali, kisha ni Hassan, kisha ni Husayn, kisha ni Ali bin Husayn, kisha ni Muhammad bin Ali, kisha ni Jafar bin Muhammad, kisha ni Musa bin Jafar, kisha ni Ali bin Musa, kisha ni Muhammad bin Ali, kisha ni Ali bin Muhammad, kisha ni Hassan bin Ali, kisha ni Muhammad bin Hassan (Mahdi)..".

("Kifayatul Athar" na rawdhatul ahbab, vya Hafidh Jamaluddin Muhaddith).

الد عاء حفضا إيمان

رَضِيْتُ بِاللّٰهِ رَبًّا وَّبِمُحَمَّدٍ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَآلِهٖ نَبِيًّا وَّبِالْإِسْلَامِ دِيْنًا وَّبِالْقُرْآنِ كِتَابًا وَّبِالْكَعْبَةِ قِبْلَةً وَّبِعَلِيٍّ وَّلِيًّا وَّإِمَامًا وَّبِالْحَسَنِ وَبِالْحُسَيْنِ وَعَلِيِّ بْنِ الْحُسَيْنِ وَمُحَمَّدِ بْنِ عَلِيٍّ وَجَعْفَرِ بْنِ مُحَمَّدٍ وَّمُوْسٰى بْنِ جَعْفَرٍ وَعَلِيِّ بْنِ مُوْسٰى وَمُحَمَّدِ بْنِ عَلِيٍّ وَّعَلِيِّ بْنِ مُحَمَّدٍ وَّالْحَسَنِ بْنِ عَلِيٍّ وَّالْحُجَّهِ بْنِ الْحَسَنِ صَلَوَاتُ اللّٰهِ عَلَيْهِمْ أَئِمَّةً اَللّٰهُمَّ إِنِّيْ رَضَيْتُ بِهِمْ أَئِمَّةً فَارْضِنِيْ لَهُمْ إِنَّكَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ.

SHUKRANI

Kitabu hiki kiliandikwa kwa lugha ya Urdu na Mtukufu Saiyadul Ulama Maulana Sayyid Ali Naqi Saheb, Mujtahid wa Chuo Kikuu cha Lucknow, Uhindi.

Kimetafisirwa kwa lugha ya Kiingereza na Sayyid Hashim Raza Rizvi, B.A., B.T., Yadgar-e-Husaini, H.S., Allahabad, Uhindi, na kutolewa na Imamia Mission, Lucknow, U.P., Uhindi.

Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kutoka hiyo tafsiri ya Kiingereza na Marehemu Bwana L.W. Hamisi Kitumboy (aliyekuwa Muballighi Mkaguzi wetu) na kikachekiwa na kusahihishwa na Mwalimu Dhikiri (Zakir Ali) U.M. Kiondo, Edita wa "*Sauti ya Bilal*".

UTANGULIZI

Ni jambo la kawaida kwa watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) kwamba ulikuwepo mfululizo wa watu kumi na wawili ambao kila mmoja wao alipata ukamilifu na utakatifu wa maisha. Watu hawa ni wale Maimamu kumi na wawili. Neno "Imamu" maana yake ni Kiongozi na ni mtu huyo tu aliyepata ukamilifu katika kila jambo linalohusu maisha ya mwanadamu awezaye kuwa mfano wa kufuatawa na watu wengine ili waweze kupata wokozi.

Kitabu hiki kinahusu maisha ya mwanadamu awezaye kuwa mfano wa kufuatwa na watu wengine ili waweze kupata wokozi.

Kitabu hiki kinahusu maisha ya Imamu wa tano wa hao Maimamu kumi na wawili.

JINA NA NASABA YAKE

Yeye amechukua jina la Mtukufu Mtume (s.a.w.) la Muhammad. Jina lake la Heshima lifahamikalo sana ni lile la Baqir. Imamu Muhammad Baqir (a.s.) ndiye Imamu pekee ambaye nasaba yake ya upande wa baba na wa mama zote zinatoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.). Baba yake ni Imamu Ali Zainul Abidiin (a.s.) Imamu wa nne, mwana wa Imamu Husain (a.s.) mjukuu mdogo wa Mtukufu Mtume (s.a.w.). Mama yake alikuwa Bibi Ummi Abdallah, binti yake Imamu Hasan (a.s.), mjukuu mkubwa wa Mtukufu Mtume (s.a.w.).

KUZALIWA KWAKE

Alizaliwa katika siku ya Ijumaa tarehe 1 Rajab mwaka wa 57 Hijiriya, miaka saba baada ya kifo cha Imamu Hasan Al-Mujtaba (a.s.), wakati Imamu Husain (a.s.) alipokuwa akipitisha maisha yake kimya kimya na wakati ambao muda ulikuwa ukiendelea kuzaa sababu za masaibu ya Karbala. Wakati huu ulikuwa mgumu sana kwa marafiki wa Dhuria wa Mtukufu (s.a.w.) na wafuasi wa Hadhrat Ali bin Abi Talib (a.s.) waliokuwa wakiwindwa ili wakatwe vichwa vyao au wasulubiwe. Kuzaliwa kwa mtoto huyu kulikuwa katika muda huu wa mfululizo wa matukio yalioongoza kwenye masaibu ya Karbala.

MASAIBU YA KARBALA

Imamu Muhammad Baqir (a.s.) alipokuwa na umri wa miaka mitatu, babu yake Imamu Husain (a.s.) alitoka Madina kwenda Iraq na Imamu Baqir (a.s.) alifuatana naye na alipata shida zote za safari hiyo ndefu. Imamu Husain (a.s.) na wafuasi wake waliponyimwa maji, Imam Baqir (a.s.) alikuwa mmoja wa wale

waliotaabika kwa ukosefu wa maji, na hakika ilimbidi afe kiu tangu tarehe saba ya mwezi wa Muharram. Lilikuwa penzi la Mwenyezi Mungu kuwa Imamu Muhammad Baqir (a.s.) hakuletwa katika uwanja wa vita wakati mtoto wa umri wa miezi sita, Bwana Ali Asghar (a.s.) alipotolewa mhanga. Ilikuwa Nyororo ya Uimamu iendelezwe kupitia baba yake na yeye, sawa na ilivyokuwa kwamba, baba yake, Imamu Ali Zainul Abidiin alikuwepo hapo Karbala lakini maisha yake hayakutolewa mhanga, vivyo hivyo Imamu Baqir (a.s.) nae alipata taabu zote lakini maisha yake yaliokolewa. Alijionea mwenyewe wakati babu yake akienda kwa mara yake ya mwisho kwenye uwanja wa vita baada ya kumchukua Bwana Ali Asghar na kisha mtoto huyo hakurudi. Aliona jinsi farasi mwaminifu wa Imamu Husain (a.s.) alivyorudi bila ya kitu chochote mgongoni mwake. Aliona jinsi mahema yalivyochomwa, jinsi walivyonyang'anywa vitu vyao na jinsi watoto na wanawake walivyotoka hema hili kwenda lile hadi mahema yote yalipoungua na wakati huo iliwabdi watoke nje bila ya "Hijaab" (shungi). Jinsi mtoto huyu alivyohisi katika masaibu hayo, hakuna mtu awezaye kujua.

Kisha baada ya tarehe 11 ya Muharram aliwaona mama yake, shangazi zake, na nyanya zake wakiwa mateka na kama mikono ya Bibi Sakinah (binti mdogo wa Imamu Husain a.s.), aliyekuwa na umri wa miaka minne wakati huo ingeliweza kufungwa katika kamba ile iliyofungiwa mikono ya wale mabibi wengine, basi hata shingo ya Imamu Baqir bila shaka nayo vile vile ingelifungwa katika kamba hiyo.

Vile vile aliona jinsi baba yake alivyokuwa akizirai karibuni kwa siku yote ile ya masaibu ya Karbala na jinsi alivyochukuliwa mateka kutoka Karbala hadi Kufah, akiwa kiongozi wa mateka na kutoka Kufah hadi Dameski. Aliona jinsi alivyolazimishwa kutembea kwa miguu mwendo mrefu (bila ya huruma) ingawa alikuwa mgonjwa, na jinsi miguu yake ilivyofungwa katika tumbo

la ngamia ili asianguke, aliona jinsi shingo yake ilivyofungwa minyororo, na jinsi alivyotiwa pingu mikononi mwake na jinsi miguu yake ilivyofungwa. Kwa hakika mambo haya yalijenga fikara mbaya sana moyoni mwa Imamu huyu ambazo zilidumu maishani mwake mwote.

KULELEWA KWAKE

Maisha yake ya baada ya masaibu ya Karbala aliyapitisha chini ya ulinzi wa baba yake, Imamu Ali Zainul Abidiin (a.s.) aliyekuwa akiishi maisha ya amani, shwari na maisha ya kujitenga mbali na ghasia za ulimwengu. Alikuwa akisali au akiomboleza kwa kifo cha baba yake. Tangu mwaka wa 61 Hijiriya hadi mwaka 95 Hijiriya, Imamu Baqir (a.s.) alikuwa akiyachunguza maisha ya baba yake na alikuwa akijifunza misingi iliyoyaongoza maisha ya watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.)

KIFO CHA BABA YAKE NA JUKUMU LA UIMAMU

Imamu Muhammad Baqir (a.s.) alikuwa na umri wa miaka 38 wakati baba yake, Imamu Ali Zainul Abidiin (a.s.) alipofariki. Kabla ya kufariki kwake Imamu Ali Zainul Abidiin (a.s.) alimpa Imamu Muhammad Baqir (a.s.) kasha la vitabu vya elimu ya dini na akawakusanya wanawe wote na kuwaweka chini ya ulinzi wa Imamu Baqir (a.s.) ambaye alikuwa Imamu wa Tano wa mfululizo huu mtakatifu wa Maimamu waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu.

HALI YA WAKATI HUO

Wakati huu serikali ya Ukoo wa Bani Umayyah ilikuwa yaelekea kuanguka. Udhalimu wao na hasa msiba wa Karbala vimeuangaza

ulimwengu wa Kiislamu kiasi cha kutosha kuhusu tabia zao. Hata Yazid mwenyewe baada ya masaibu ya Karbala aliathiriwa sana na kosa alilolifanya na mwanawe Muawiyah alikuwa akiyalaumu sana hadharani matendo ya baba yake na babu yake, na alikataa kutawala baada ya baba yake. Basi vipi watawala waliofuatia wasiwaze kuyajali mambo ya wakati ule wakati walipokwisha kuona jinsi watu walivyokuwa wakiiasi serikali yao. Hivyo Imamu Muhammad Baqir (a.s.) aliweza kukaa kwa amani kidogo na kutokana na amani hiyo aliweza kufanya zaidi kuhusu uenezaji wa Uislamu kuliko Maimamu wengine waliomtangulia.

KAZI YAKE YA UALIMU WA SHERIA YA MWENYEZI MUNGU

Kijito cha Elimu ya Mwenyezi Mungu kilichofungwa kwa muda mrefu, kilipopata nafasi ya kutosha kilianza kutiririka kwa mwanga ulioonekana kwa nadra sana katika historia ya mafundisho ya Sheria za Mwenyezi Mungu. Watu wengi sana walimjia ili wasome, wakiwemo wale waliokuwa bado kujiambatanisha na Maimamu kuhusu imani zao, kiasi ambacho aliitwa "Baqir" (mtu adhihirishaye vitu vilivyojificha) kwa kuwa alifafanua mambo mengi ya Elimu ya Kidini ambayo kama si kwa kuyaeleza kwake yasingelifahamika kwa Waislamu.

Wanachuoni wa Kisunni kama vile Zahri, Imamu Auza-i-ata bin Juraih na Qadhi Hafs bin Ghiyas ni miongoni mwa wanafunzi wake.

KUENEZA ELIMU ZA KIDINI

Katika zama zake Imamu Muhammad Baqir (a.s.) uenezaji wa Elimu ya Kidini ambayo watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (a.s.)

walikuwa walinzi wake, ilidumishwa. Wanafunzi wake mashuhuri waliandika vitabu vingi vya elimu mbali mbali. Hapa tunawataja wachache kati ya wanafunzi hao:-

1. Bwana Aban bin Taghlib. Inakubalika kuwa Bwana huyu alikuwa mwnachuoni mkuu wa "Tajwid" (Usomaji wa Qur'ani Tukufu na Elimu ya Lugha). Alikuwa mtu wa kwanza kuandika kitabu kinachohusu "Gharib-ul-Qur'an" (maneno magumu ya Qur'ani Tukufu). Alifariki mnamo mwaka wa 141 Hijiriya.

2. Bwana Abu Jaafar Muhammad bin Hasan Bin Abi Sarah Rawasi. Alikuwa mwanachuoni mkubwa wa Elimu ya Usomaji, Tafsiri ya Qur'ani Tukufu na Sarufi. Aliandika vitabu vitano vikiwemo "Kitab-ul-Faisal" na "Ma'ani-Al-Qur'ani". Bwana huyu alifariki mnamo mwaka wa 101 Hijiriya.

3. Bwana Abdallah bin Maimun Aswadul Qidah. Vitabu vyake alivyoviandika ni pamoja na kitabu kinachohusu Wito wa Mtukufu Mtume (s.a.w) kuwaita watu kwenye Uislamu na kingine kuhusu "Pepo na Mtoto". Bwana huyu alifariki mnamo mwaka wa 105 Hijiriya.

4. Utaiyah bin Said Aufi. Aliandika Tafsiri ya Qur'ani yenye majalada matano. Alifariki mnamo mwaka wa 111 Hijiriya.

5. Bwana Ismail bin Abdul Rahman Al-Suddi Al-Kabir. Huyu ni Mfasiri mashuhuri sana wa Qur'ani Tukufu anayetajwa na wafasiri wote wa Kiislamu kwa jina la Suddi. Alifariki mnamo mwaka wa 127 Hijiriya.

6. Bwana Jair bin Yazid Jufi. Bwana huyu alikariri Hadithi elfu hamsini za Mtukufu Mtume (s.a.w.) na kufuatana na wasemavyo baadhi ya watu, bwana huyu alikariri hadithi elfu

sabini. Jambo hili limeelezwa katika "Sahih" ya Bwana Muslim. Aliandika vitabu vichache hivi juu ya tafsiri ya Qur'ani, Hadithi na sheria za Kiislamu (Fiqah). Alifariki Mnamo mwaka wa 128 Hijiriya.

7. Bwana Ammar bin Muawiah Duhni. Aliandika kitabu cha Sheria za Kiislamu (Fiqah). Alifariki mnamo mwaka wa 133 Hijiriya.

8. Bwana Salim bin Hafsa Abu Yunus Kufi. Bwana huyu yu mwandishi wa kitabu cha Fiqah. Alifariki mnamo mwaka wa 137 Hijiriya.

9. Bwana Abdul Mu'min bin Qasim Abu Abdallah Ansari. Aliandika kitabu cha Fiqah. Bwana huyu alifariki mnamo mwaka wa 147 Hijiriya.

10. Bwana Abu Hamza Thumali. Bwana huyu aliandika Tafsiri ya Qur'ani Tukufu, Kitabu kiitwacho "Kitabul-ul-Nawadir" na kingine kiitwacho "Kitabul-Zuhd". Alifariki mnamo mwaka wa 150 Hijiriya.

11. Bwana Zuarah bin A'yan. Bwana huyu alikuwa mwanachuoni mkuu wa Kishia na vitabu vyake vingi alivyoandika kuhusu Lugha, Fiqah na Hadithi bado vinapatikana hadi leo. Alifariki mnamo mwaka wa 150 Hijiriya.

12. Bwana Muhammad bin Muslim. Bwana huyu alijifunza Hadithi elfu thelathini kwa Imamu Baqir (a.s.) na aliandika vitabu vingi, kimojawapo kinaitwa "Chahar Sad Mas'ala dar Abwab-i-Halal-Haram". Alifariki mnamo mwaka wa 150 Hijiriya.

13. Bwana Yahya bin Qasim Abu Baseer Asadi. Bwana huyu

alikuwa na cheo kikubwa sana miongoni mwa wanafunzi wa Imamu Baqir (a.s.). Aliandika kitabu kiitwacho "Munasik-i-Haj" na kingine kiitwacho "Kitab yaum wa Lailah". Alifariki mnamo mwaka wa 150 Hijiriya.

14. Bwana Ishaq Qummi. Bwana huyu alikuwa mwandishi wa kitabu fulani cha Fiqah.

15. Bwana Ismail Bin Jabir Khath'ami Kufi. Bwana huyu aliandika vitabu kadhaa vya Hadithi na kitabu kimoja cha Fiqah.

16. Bwana Ismail bin Abdul Khaliq. Bwana huyu alikuwa na cheo kikubwa na aliandika kitabu cha Fiqah.

17. Bwana Barad-al-Azadi bwana huyu aliandika kitabu cha Fiqah.

18. Bwana Haris bin Mughirah. Bwana huyu vile vile aliandika kitabu cha Fiqah.

19. Bwana Huzaif bin Mansur Khuzai. Yeye naye aliandika kitabu cha Fiqah.

20. Bwana Hasan bin Al-Sariy Al-Katib. Vile vile aliandika kitabu kimoja.

21. Bwana Husain bin Abi Fakhta. Bwana huyu aliandika kitabu kinachoitwa "Kitab-ul-Nawadir".

22. Bwana Husain bin Hammad Abdi Kufi. Aliandika kitabu kimoja.

23. Bwana Husain bin Musab Bijali. Vile vile aliandika kitabu kimoja.

24. Bwana Hamad bin Abi Talha. Bwana huyu aliandika kitabu kimoja.

25. Bwana Hamzah bin Hamran bin Ayan. Bwana huyu alikuwa mwana wa nduguye Bwana Zurarah bin A'yan (tuliye mtaja hapo juu katika nambari 11) na huyu naye aliandika kitabu kimoja

Haya ni majina machache tu ya wanachuoni na mashehe waliojifunza elimu ya dini kwa Imamu Muhammad Baqir (a.s.), na kuzihifadhi elimu hizo katika vitabu ambavyo, pamoja na mamia hayo ya vitabu vilivyoandikwa katika zama za Imamu Jaafar As-Sadiq (a.s.) mwana na mrithi wa Imamu Baqir (a.s.) vilitoa mambo yaliyotumika kwa kuandika vitabu viitwavyo "Kafi", "Man La Yahzur", "Tahzib na Istibsar", vitabu ambavyo baadaye vilikuwa asili kuu ya Hadithi za Kishia.

TABIA ZAKE

Hata maadui wake walikiri kuwa Imamu Muhammad Baqir (a.s.) alikuwa na tabia nzuri sana. Mtu mmoja kutoka Shamu aliyekuwa akiishi mjini Madina alikuwa na kawaida ya kuja na kukaa karibu na Imamu (a.s.). Alisema kuwa ingawa yeye hakuhusiana vyo vyote vile kidamu na watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) alivutiwa sana na upole, tabia nzuri sana na hotuba za Imamu (a.s.) kiasi cha kumfanya amwendee kumsikiliza.

USHAURI WAKE KWA SERIKALI

Uongozi wa nchi ya Kiislamu ulikuwa ni haki yao hawa Maimamu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.), lakini ulimwengu

ulipozisujudia nguvu za kidunia, Maimamu hawa walijitenga na kuishi maisha ya kimya kimya na ya amani. Kufuatana na fikara za kidunia inawezekana kutegemewa kuwa katika hali kama hiyo, Maimamu hao wangeliweza kukataa kutoa ushauri au misaada mingine kwa wanyang'anyi hao wa Ukhalifa. Lakini Maimamu hawa walikuwa watu wenye tabia za kipekee kabisa. Sawa kabisa na alivyokuwa Hadhrat Ali bin Abi Talib (a.s.) kuwa alikuwa akitoa msaada wa mara kwa mara kwa watawala wa zama zake, vile vile wale watu wengine wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) kila mara walikuwa tayari kuwasaidia watawala wa zama zao kila mara ummah au Uislamu ulipohitaji msaada wao. Katika zama za Imamu Muhammad Baqir (a.s.) hazikuwepo sarafu za Dola ya Kiislamu na badala yake zilitumika sarafu za Kirumi. Wakati wa utawala wa mfalme Walid bin Abdul Malik kulitokea kutoafikiana baina ya serikali ya Shamu na ya Urumi na serikali ya Kirumi ilitoa pendekezo lake la kutaka kuandika maneno fulani yanayoonyesha kutomheshimu Mtume (s.a.w.) katika sarafu zake. Jambo hili liliwaudhi sana Waislamu. Walid aliitisha mkutano mkubwa ambao ulihudhuriwa na watu mashuhuri wa ulimwengu mzima wa Kiislamu. Imamu Baqir (a.s.) pia alihudhuria na alishauri kuwa serikali ya Kiislamu ifue sarafu zake na katika upande mmoja wa sarafu hizo iandikwe sentensi isemayo "La Ilaha Illallah" na katika upande wa pili iandikwe sentensi isemayo "Muhammadun-Rasulullah". Wazo hilo lilikubaliwa na sarafu zilifuliwa kama alivyoshauri Imamu Baqir (a.s.)

KUSUMBULIWA KWAKE NA SERIKALI YA BANI UMAYYAH

Ingawa Imamu Muhammad Baqir (a.s.) hakuingilia mambo yoyote ya kiserikali (na ilipombidi kufanya hivyo alifanya ili kutoa ushauri kwa ajili ya kuihifadhi heshima ya Nchi ya Kiislamu, na

kwa kuombwa na serikali yenyewe), hata maisha yake ya amani na kuutumikia Uislamu wa Kweli hayakuweza kuvumiliwa na mfalme Hisham bin Abdul Malik. Hisham alimwandikia barua Gavana wake wa Madina awapeleke Dameski, Imam Baqir (a.s.) na mwanawe Imamu Jaafar (a.s.) kwa shabaha ya kutaka kuwakebehi na walipofika Dameski hakukutana nao kwa muda wa siku tatu na mnamo siku ya nne aliwaita katika baraza lake. Hisham alikuwa kaketi katika kiti chake cha enzi na askari wake walisimama kwa mstari kuumeni na kushotoni kwake. Liliwekwa dango (kitu cha kulengea shabaha) na wakuu wa baraza walikuwa wakitupa mishale yao katika dango kwa kulana. Imamu (a.s.) alipofika, Hisham alimtaka nae acheze mchezo huo wa shabaha. Kwanza Imamu (a.s.) alikataa, lakini Hisham alimshikilia afanye hivyo. Alifikiria kuwa kwa kuwa watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) walikuwa wakiishi maisha ya kujitenga kwa muda mrefu bila shaka walisahau mambo kama haya na kwa kumshikilia kufanya hivyo atakuwa anamtweza Imamu (a.s.). Hisham hakujua kuwa kila mmoja wa watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) alikuwa na uwezo kama ule wa mikono ya Hadhrat Ali (a.s.) na moyo kama ule wa Hadhrat Husain (a.s.). Imamu (a.s.) alichukua upinde na mishale mikononi mwake na baada ya kulenga shabaha alifuma mishale tisa mmoja baada ya mwingine katika njia ambayo baada ya ule mshale wa kwanza kulifuma lile dango, ile mingine minane ikafuatia kila moja ukifuma sehemu ya nyuma (yenye manyoya) ya mshale uliotangulia na kuupasuapasua. Watu wote waliokuwepo pale walimshangilia Imamu (a.s.) na Hisham alitahayari kwa yale aliyomtendea Imamu (a.s.). Kisha Imamu (a.s.) alijadiliana na Hisham kuhusu suala la Ukhalifa na Maadilifu ya watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.). Kisha Hisham alifikiria kuwa kuendelea kwa Imamu (a.s.) kukaa mjini Dameski kutawafanya watu wampende, jambo ambalo litazaa hatari kwa serikali. Hivyo Imamu (a.s.) akamruhusu arudi Madina.

KUFARIKI KWAKE

Jinsi serikali ya Shamu ilivyoyahisi maadilifu ya Imamu (a.s.) ndivyo ilivyozidi kupendelea kumwulia mbali.

Kwa ujumla, ile silaha ya kisirisiri iliyokuwa ikitumiwa na watawala wa Dameski kuyaondolea maisha matakatifu ya Watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.), ilitumika kuyaondolea maisha yake. Walimpa Imamu (a.s.) sogi lililokuwa na sumu katika matabaka ya ngozi zake, na Imamu (a.s.) alipolitumia, sumu ile ilienea mwilini mwote na ikamdhuru. Baada ya kuugua kwa siku chache hivi kwa maumivu makali alifariki mnamo tarehe 27 ya mwezi wa Dhul-Hajj (mfunguo Tatu) wa mwaka wa 114 wa Hijiriya baada ya kuishi kwa muda wa miaka hamsini na saba.

Kufuatana na alivyousia, maiti yake ilifungwa katika nguo tatu: Kwanza shuka ya nguo ya Yaman aliyokuwa akiitumia katika sala ya Ijumaa wakati wa uhai wake, pili shati alilokuwa akilivaa wakati wa uhai wake na tatu, nguo nyingine.

Alizikwa katika Kuba moja iliyokuwepo katika makaburi ya Janatul-Baqi ambamo Imamu Hassan (a.s.) na Imamu Ali Zainul Abidiin (a.s.) walizikiwa.

BAADHI YA HADITHI ZA IMAMU MUHAMMAD BAQIR (A.S.)

1. (Vitu viwili), kuridhika na umaskini huzungukazunguka moyoni mwa mtu aliyeamini (na) vinapofikia kilele cha kumtegemea Mwenyezi Mungu, huzama tena moyoni mwake.

2. Tendo jema zaidi ni kujihadhari na kila kitu kisicho cha halali na kujihadhari na zinaa.

3. Tegemea kupata kutoka kwa nduguyo sawa na kile unachompa.

4. Wakati kiburi kinapouingia moyo wa mtu yeyote, humuondolea fikara zake njema.

5. Silaha ya ubaya ni kutumia maneno mabaya.

6. Shetani hupendelea zaidi kifo cha mtu mmoja mwenye elimu kuliko vifo vya Wachamungu sabini.

7. Mtu mwenye kuamini hauamini ulimwengu, kwa maana ya kuwa u wenye kwisha; wala haoni kuwa yu huru kutokana na siku ya Kiyama, kwa maana siku hiyo itakuwa mbaya sana.

8. Enyi watu wa dunia, walio Wachamungu miongoni mwenu ndio wasaidizi wenu bora; kama mkiwasahau watakukumbukeni, na kama mkiwakumbukeni watakusaidieni. Wao ndio walinzi wa kile mnachodaiwa na Mwenyezi Mungu nao wanasimama kwa ajili ya penzi la Mwenyezi Mungu.

9. Ufikirie Ulimwengu kuwa ni mahali pa kupumzikia ambapo ulipumzikia na kisha ukaondoka; au ndoto (uliyopata kuota na) ambayo imeondoka kabisa akilini mwako bila ya kuacha kumbukumbu yoyote.

10. Imani ya mtu haiwezi kukamilika mpaka hekima ya mtu huyo ikamilike, na hiyo hekima haikamiliki mpaka mtu huyo awe anayo mambo kumi:-
    i. Ategemewe kufanya mambo mema.
    ii. Watu wasiogope lolote lile lililo baya kutoka kwake.

iii. Ajifaidie kidogo sana kutokana na maendo yake mema.
iv. Anayasamehe zaidi mabaya ya watu wengine.
v. Hakomi kumwomba Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mahitaji yake.
vi. Hachoshwi na kujitafutia elimu.
vii. Unyonge ni bora kwake kuliko utukufu.
viii. Hupendelea zaidi umaskini kuliko utajiri.
ix. Hutosheka na chakula chake cha kila siku.
x. Kila anapokutana na mtu yeyote yule hufikiria, 'Bila shaka mtu huyu yu mbora na mtenda mema kuliko mimi.

11. Utawaona watu wa aina mbili, aliye mwema kuliko wewe na aliye Mchamungu zaidi; na mwingine aliye chini yako katika wema na Uchamungu. Unapokutana na yule aliye mbora, kuwa mtiifu mbele yake kwa maana ana cheo kikubwa kuliko chako, na unapokutana na yule aliye na cheo cha chini kuliko chako mfanye kuwa juu yako kwa maana anaweza kuwa na matendo mema ya kisirisiri. Mtu afanyaye hivyo huwa mtu bora zaidi katika zama zake.

12. Usijirafikishe na watu hawa wane:-
    i. Mpumbavu
    ii. Bahili
    iii. Mwoga
    iv. Mwongo

    Mpumbavu atataka akufanyie mazuri lakini atakudhuru. Bahili kila mara atataka kupata vitu kutoka kwako. Mwoga kila mara atajaribu kukuepuka wewe na wazazi wake. Hakuna mtu yeyote yule awezaye kuthibitisha maneno ya mtu mwongo.

13. Wako watu wa aina tatu wasomao Qur'ani. (Wa kwanza ni) yule aisomaye Qur'ani ili kujiunga na watu matajiri, na hivyo

kuwaghilibu watu wengine. Mwingine husoma Qur'ani kwa ajili ya kuyahifadhi maandishi yake na kuiua ile roho yake. Na mtu wa tatu husoma Qur'ani kwa ajili ya kuzikabili ghasia za mwili, hivyo haisomi usiku. Hupenda kuisoma wakati wa mchana, kuirudia tena msikitini na huendelea nayo kitandani. Mwenyezi Mungu humwondolea maovu yake, humwondolea maadui, (na) huleta mvua anapoiomba. Watu wa aina hii ni wachache sana.

14. Siku moja Mkristo mmoja aitwaye Abdul Ghaffar, alikwenda kwa Imamu (a.s.) na kuzungumza naye mazungumzo yafuatayo:-

Abdul Ghaffar: Ni tendo gani lililo bora zaidi?

Imamu (a.s.): Yule aliye mvumilivu.

Abdul Ghaffar: Ni yupi aliye na Imani ya kweli?

Imamu (a.s.): Yule aliye na tabia nzuri zaidi

Abdul Ghaffar: Ni jihadi ipi iliyo nzuri zaidi.

Imamu (a.s.): Ni ile ambayo ndani yake miguu ya farasi wa askari imekatwa na damu ya askari huyo imemwagika.

Abdul Ghaffar: Ni sala gani iliyo bora zaidi?

Imamu (a.s.): Ni ile iliyo na Qunuut ndefu sana (Sala ya mtu binafsi wakati wa Sala).

Abdul Ghaffar: Ni wema upi ulio mzuri zaidi?

Imamu (a.s.): Kujihadhari na vitu visivyo halali.

Abdul Ghaffar: Nini imani yako kuhusu kwenda kuonana na wafalme?

Imamu (a.s.): Si jambo zuri kwako kulifanya.

Abdul Ghaffar: Ninataka kwenda kuonana na mfalme Ibrahimu bin Walid, mfalme wa Shamu. Je, unayo sababu maalum ya kulikatalia jambo hilo?

Imamu (a.s.): Kwenda kuonana na wafalme hukuongoza kwenye mambo matatu, kuvipenda vitu vya kidunia, kuki sahau kifo na kutotosheka na kile Mwenyezi Mungu anachotuandalia.

Abdul Ghaffar: Kwa sababu ya familia kubwa niliyonayo, ningependa kwenda huko (Shamu) ili nikapate faida fulani.

Imamu (a.s.): Sisemi kuwa uwe unajinyima vitu hata vilivyo halali, bali nakutaka uwe Mchamungu.

ISBN: 9976 956 03 7



Kimetolewa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P 20033
Dar es Salaam